

MINUTE SHEET

DOKEZO
No.

KUTOKA : Mkurugenzi Mtendaji
Kituo cha Uwekezaji Tanzania
DAR ES SALAAM

KWENDA : Katibu Mkuu
Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
DODOMA

Prof. Longinus K. Rutasitara
Mwenyekiti wa Bodi – TIC
DAR ES SALAAM

Wafanyakazi Wote – TIC

TAREHE : 29 Agosti, 2018

YAHUSU : **TAARIFA YA SAFARI: BEIJING - CHINA**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Napenda kuwajulisha kuwa ninaambatana na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Tanzania ambapo pamoja na mambo mengine atamwakisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) utakaofanyika Beijing, China. Aidha, lengo kuu la ushiriki wa Kituo katika ziara hiyo, ni kuwasilisha mada kuhusu fursa za uwekezaji wa viwanda nchini pamoja na aina mbalimbali za vivutio kwa wawekezaji wenye nia ya kufanya uwekezaji nchini, kupitia Jukwaa la Biashara lililoandaliwa na Taasisi ya China Machinery Industry Federation. Jukwaa hili ni mahususi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa viwanda kutoka China kuja Tanzania.

MINUTE SHEET

DOKEZO
No.

Ziara hii itaanza tarehe 30 Agosti hadi 16 Septemba, 2018. Ninatarajia kurejea nchini tarehe 17 Septemba, 2018.

Kibali chenye **Kumb. Na. 1968-V1535438960-928244** kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi -Ikulu cha tarehe 29 Agosti, 2018 chahusika.

Katika safari hiyo nitaambatana na Bw. George Mukono – Afisa Mwandamizi – Uhamasishaji/Huduma kwa Uwekezaji/Msaidizi wa Mkurugenzi Mtendaji.

Nitakapokuwa safarini, Bw. John Mathew Mnali, Mkurugenzi katika Kurugenzi ya Uhamasishaji Uwekezaji atakaimu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji.

Nawatakia kazi njema.



Geoffrey I. Mwambe
MKURUGENZI MTENDAJI

Nakala: Bw. John Mathew Mnali
Mkurugenzi
Kurugenzi ya Uhamasishaji Uwekezaji
DAR ES SALAAM

Wakuu Wote wa Idara
Kituo cha Uwekezaji Tanzania
DAR ES SALAAM